# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
# VETA -KIPAWA CHUO CHA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO


Simu : +255 -22-2843360/3
Nukushi: +255- 22-2843364

S.L.P 40040
DAR ES SALAAM
Barua pepe: kict@veta.go.tz
Tovuti: www.vetakipawa.ac.tz


---

TAREHE:.............................

JINA KAMILI LA MWANAFUNZI:.............................................................................................

ANUANI:.............................................................................................................................

NA. YA SIMU:.....................................................................................................................

BARUA PEPE:......................................................................................................................

**YAH: KUCHAGULIWA KUENDELEA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KATIKA CHUO CHA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO-VETA KIPAWA KWA MWAKA WA MASOMO 2024.**

**MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI KABLA YA KULIPA ADA**

## A. UTANGULIZI

1. Unafahamishwa kwamba umepata nafasi ya kujiunga na mafunzo katika fani ya ..........................................................daraja la 1[ ].
2. Mafunzo yatachukua muda wa mwaka **mmoja kwa (daraja la 1)**.
3. Chuo kitafunguliwa rasmi Tarehe: **15 Januari, 2024** saa 1: 30 asubuhi.
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari kuwa unayo afya njema ya kumudu mafunzo katika fani uliyoomba, kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa nane (8)

5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi hiyo ya mafunzo, mara upatapo tu barua hii **Jaza kiambatanisho ukurasa wa tisa (9).**

B. **VIFAA MUHIMU**

Unatakiwa kununua mahitaji yafuatayo kwa matumizi yako chuoni:-

1. Mashati mawili meupe ya Tetron (mikono mirefu).
2. Suruali mbili rangi ya bluu ambazo sampuli ya kitambaa utaipata chuoni.
3. Viatu vya ngozi rangi nyeusi na soksi pea mbili nyeusi.
4. Koti mbili (2) za maabara rangi nyeupe.
5. Madaftari makubwa (10) na daftari (1) lisilo na mistari.
6. Vifaa vya hesabu na kuchorea (mathematical set).
7. Kijitabu cha logi (mathematical tables)
8. Safety boots kwa ajili ya kujifunzia karakana.

C. **MAHITAJI MBALIMBALI,** Kama yanavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:-

| S/No | Maelezo | Malipo |
|---|---|---|
| 1. | Fomu ya kujiunga | 5,000 |
| 2. | Ada | 60,000 |
| 3. | Ada ya mtihani daraja la I | 25,000 |
| 4. | Pesa za tahadhari | 10,000 |
| 5. | Nembo | 4,000 |
| 6. | Flana | **20,000** |
| 7. | Kitambulisho | **10,000** |
| 8. | Huduma ya kwanza | **15,000** |
| | **JUMLA** | **149,000** |

## D. ADA NA UTARATIBU WA KULIPA

Ada ya mafunzo ni Tshs.**60,000/= na fomu ni shilingi 5,000/=** kwa mwaka ukijumulisha na gharama za mahitaji mengine muhimu kwa daraja la kwanza ni Tshs.**84,000/=** Hivyo kufanya jumla kuwa **Tsh.149,000/=.**

1. Unapaswa kulipa ada yote mara moja tu, wakati unapofika chuoni, Jumla ya malipo yote kwa mwaka mzima **ni shilingi Laki Moja na arobaini na Tisa Elfu (Tsh.149, 000/=)** pesa hii ilipwe kupitia mfumo wa GePG ambapo utapewa control number inayopatikana katika ofisi za uhasibu na utaipeleka benki. Baada ya malipo kufanyika benki utapewa risiti nayo utaiwasilisha ofisi ya uhasibu ili uweze kupatiwa risiti ya malipo.
2. Chuo hakitapokea malipo ya fedha taslimu yahusuyo Ada na gharama zingine. Malipo yote yalipwe benki ya **CRDB Tawi lolote Nchini, Malipo yafanyike mara tu unapojiunga na chuo.**

**Hakikisha stakabadhi ya malipo ya benki ina jina kamili la mwanafunzi.(Jina liwe ni lile lililopo kwenye vyeti vyako vinavyotumika shuleni).**

### NB:-BIMA YA AFYA

*1. Ni lazima uje na Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu la sivyo hutapokelewa chuoni.*

## E. MASHARTI YA KUSAJILIWA

Ili usajiliwe lazima ukidhi vigezo vifuatavyo:-

1. Uthibitisho wa kufaulu wa kidato cha nne mwanafunzi aje na kivuli cha cheti cha kumaliza sekondari (academic certificate)
2. Kulipa na kuwasilisha stakabadhi ya malipo ya benki mapema ili uweze kusajiliwa (wiki moja kabla ya siku ya kufungua chuo).
3. Unatakiwa kusaini kukubali kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua hii, ukurasa wa tano (5).
4. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kufungua na kuanza mafunzo.
5. Nafasi yako **itapotea** iwapo utashindwa kufika kwa muda wa wiki mbili baada ya chuo kufunguliwa.
6. Fedha ikishalipwa hairudishwi.

**KUMBUKA:**
**Chuo kina mamlaka ya kusitisha mafunzo yako iwapo hautafikia kiwango cha kufaulu kilichowekwa ama utakapogundulika kuwa ni mtovu wa nidhamu ama kukiuka masharti ya chuo.**

**"Maelezo mengine utapewa ufikapo chuoni".**

**Kwa niaba ya chuo cha TEHAMA - VETA KIPAWA**

..........................................................

Mha.Sospeter Dickson Mkasanga
**MKUU WA CHUO.**

## SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA CHUO CHA TEHAMA VETA KIPAWA (KICTC)

ILI UWEZE KUFANYA MAFUNZO YATAKAYOENDESHWA KATIKA CHUO CHA TEKINOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO, UNAPASWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:-

### 1. MAHUDHURIO

(a) Unatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:30 asubuhi. Hii inamaana ifikapo saa 1:30 wanafunzi wote muwe mmeshafika chuoni. Hatua kali ya kinidhamu itachukuliwa kwa wachelewaji.

(b) Hutakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote ile, bila ya kuruhusiwa na (Mkuu wa sehemu au mwalimu wa darasa).

(c) Upatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe nilazima habari/taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.

(d) Mahudhurio chini ya 85%, utakosa sifa ya kuhitimu na hutaruhusiwa kufanya mtihani wa Taifa.

### 2. MAVAZI

(a) Sare ya chuo ni suruali ya Blue na shati Jeupe mikono mirefu/T-shirt (Flana). Sare hiyo uivae wakati wote, uwapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa na liwe na nembo ya VETA. Flana uivae siku ya Jumatano na Ijumaa tu.

(b) Ovakoti ulivae wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(c) Viatu vyenye visigino virefu, kandambili au viatu vya wazi (Sandals) huruhusiwi kuvivaa uwapo chuoni.

### 3. USAFI WA MWILI

(a) Huruhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili, mkufu na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.

(b) Nywele Kwa Wavulana:-

i) Uzikate ziwe fupi sana, Kipara, Panki huruhusiwi kabisa.

ii) Huruhusiwi kufuga ndevu (Sharubu, sharafa, ndevu kidevuni na kionja mchuzi).

(c) Nywele Kwa Wasichana

i) Uzikate zisiwe fupi sana, Kipara, Panki huruhusiwi kabisa au

ii) Zisuke kwa mistari ya kurudi nyuma.

(d) Huruhusiwi kufuga wala kupaka rangi kucha.

### 4. USAFI WA MAZINGIRA

(a) Unatakiwa kuhakikisha maeneo yote yanayokuzunguka ni masafi, kwa kuokota uchafu wowote utakaouona na kuweka sehemu husika za kutupa taka.

(b) Ni marufuku kushika au kukanyaga kuta za jengo; uwapo karakana au darasani ama nje.

(c) Ni marufuku kuingia darasani au karakana na aina yoyote ya **kimiminika**, **chakula**, **bazoka** nk.

(d) Huruhusiwi kupita kwenye eneo la katikati (Corridor) ya Ofisi za Utawala pindi uendapo kantini isipokuwa unapokuwa nashida ya kiofisi.

(e) Huruhusiwi kukatisha katika sehemu za **bustani za maua**au **sehemu zilizopandwa nyasi**, unatakiwa kutumia njia husika (Pavement).

## 5. WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:

(a) Vitendo vyovyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi umeiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzako, hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa chuoni.

**NB:** Kifaa au mali yeyote isiyo ya chuo unatakiwa uiandikishe na ikaguliwe getini kwa walinzi kabla ya kuingia darasani na baada ya kutoka darasani.

(b) Usafi wa maeneo yote ya chuo ni wajibu wa kila mwanafunzi hivyo unawajibika kila wakati kutunza bustani, maeneo yote ya ndani na nje ya chuo kuwa safi daima.

# VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

## VETA-KIPAWA INFORMATION AND COMMUNICATION TECHNOLOGY CENTRE (KICTC)

Telephones: +255 -22-2843360/3

Telefax: +255- 22-2843364

P.O. BOX 40040

DAR ES SALAAM

E- mail: kict@veta.go.tz

Website: www.vetakipawa.ac.tz


The medical Office

Date.........................

...........................................

...........................................

...........................................

...........................................

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine the above name candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/ an

i) Eyesight
ii) Hearing
iii) Asthma
iv) Epilepsy
v) Other serious disease

## MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above named and consider that she/he is physically for training as above.

Signature ..............................

Date ............................

## KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

(a) **MWANACHUO**

Mimi.......................................................................... ninakubali nafasi/mafunzo katika fani niliyopangiwa/niliyoomba na ninaahidi kufuata na kutii taratibu na sheria zilizowekwa na chuo kwa muda wote wa mafunzo hapo chuoni.

(b) **MDHAMINI**

Mimi.......................................................S.L.P...........................................................................

Ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani aliyopangiwa na ninathibitisha kuwa nitamdhamini aliyetajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za mafunzo (ada) n.k.

Pamoja na nauli wakati wa kwenda na kurudi kwa kipindi chote cha mafunzo. Ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani aliyopangiwa.

Sahihi............................................ Tarehe......................................